

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina.

# Waziri Mpina 'alivyowazawadia' Krismasi na Mwaka Mpya Kagera

**Na Joseph Sabinus**

JUZI tulikuwa Sikukuu ya Krismasi iliyofuatiwa na Siku ya kufungua zawadi (Boxing Day) jana. Wakristo nchini waliungana na wenzao duniani kuadhimisha kumbukumbu ya kuzaliwa kwa Mkombozi wa Ulimwengu, Yesu Kristo yapata miaka 2000 iliyopita.

Miongoni mwa watu walioshereheka sikukuu hiyo ya Krismasi na hata sikukuu ijayo ya kuaga mwaka 2019 na kuanza mwaka mpya wa 2020 kwa furaha zaidi, ni wakazi wa Mkoa wa Kagera ambao Waziri Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, 'amewapa zawadi' ya kufungia mwaka na kuanza mwaka mpya.

Hii ni zawadi muhimu na msingi wa maendeleo ya jamii yoyote ama iwe kiroho, au kimwili. Zawadi ya amani.

Katika maadhimisho hayo maaskofu na viongozi mbalimbali wa Kikristo wakiwamo wachungaji, mapadri na wainjilisti katika nyakati na maeneo tofauti, walisisitiza mintarafu tunu ya amani kwa mtu mmoja mmoja, familia, jamii na taifa kwa jumla.

Kwa mfano, Askofu wa Jimbo Katoliki la Shinyanga, Liberatus Sangu, alinukuliwa akisema katika mkesha wa Krismasi jimbo Shinyanga kuwa, uchu wa madaraka na tamaa ya utajiri vinachochea mifarakano ndani ya familia na mauaji kwa watu wasio na hatia wakiwamo wazee, watu wenye ulemavu wa ngozi (ualbino), watoto na wazee mambo aliyosema yanahatarisha amani nchini.

Katika ibada ya kwanza ya Krismasi juzi, Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Fredrick Shoo akiwa Usharika wa Moshi Mjini alilitia uzito wa tunu ya amani kwa Watanzania akisema: "Tuache kuwatesa wanadamu wenzetu, tuache kufurahia kuwatesa wengine wasio na hatia, iwe ni katika nyumba zetu..."

Akaendelea: "Kuna watu wanateseka sana katika nyumba zao ... Kuna watu wanateswa. Kuna watu wanateswa, watoto, wake kwa waume wanateswa. Namaliza amani anayotuletea Yesu Kristo katika Krismasi ipo katika nyumba zetu, ipo katika jamii yetu kweli?"

Naye Askofu wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Kati, Dickson Chilongani akasema anachukizwa na tabia ya baadhi ya wanasiasa kutumbilia kwa waganga wa kienyeji kipindi cha uchaguzi kinapowadia sambamba na tabia ya baadhi ya watu kugeuza sikukuu ya Krismasi kuwa ya kuchafua amani ambayo Mungu amemtunuku mwanadamu.

Akasema: "Kipindi cha Krismasi si cha kuchafua amani, bali kuimarisha, kujenga na kudumisha amani kwa jamii kwa kuepuka vitendo viovu na migogoro."

Naye Mchungaji Kiongozi wa Kanisa la Mlima wa Moto, Getrude Rwakatare juzi alinukuliwa akisema Krismasi ni kipindi cha kuenzisha amani kwa watu wakiwamo ndugu, jamaa, marafiki, majirani na walioogombana na kuhamiana kupitia msamaha, maridhiano, suluhu na kujenga undugu mpya wenye nguvu zaidi.

Wakati Watanzania wakisherehekea sikukuu hiyo kuelekea mwaka mpya wa 2020, Serikali ya Tanzania kupitia kwa Waziri Luhaga Mpina inayotekeleza agizo la Rais wa Awamu ya Tano, John Magufuli, imewapa zawadi ya amani wakazi wa Mkoa wa Kagera baada ya kumaliza mgogoro uliodumu kwa takriban miaka 15.

Kwangu mimi, kitendo cha Waziri Mpina kuamua vijiji vilivyokuwa ndani ya ranchi kubaki na kuendelea na shughuli za kilimo na ufugaji ni zawadi kubwa ya Krismasi kuelekea mwaka mpya iliyotolewa na waziri huyo kwa wakazi wa Kagera kwa niaba ya serikali chini ya Rais John Magufuli.

Zawadi ya Mpina kwa wananchi hao ambao sasa wanaanza wanawaza urithi wa tunu ya amani mauy... baada ya kumaliza mgogoro wa ardhi baina ya wananchi na Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO), ni utekelezaji wa agizo la Rais Magufuli la kumegua maeneo ya serikali ya ranchi na kuwagawia wananchi wa vijiji vilivyokuwa ndani ya ranchi hizo, badala ya kuwataka wahame.

Akazungumza katika mkutano wa hadhara katika

# Japan provides 4.2bn/- for TAFICO's revival

By HILDA MHAGAMA

AS plans are underway to revive the Tanzania Fishing Corporation (TAFICO), the government of Japan has provided a financial grant of 4.2bn/- to support the implementation of the project.

The Permanent Secretary in the Ministry of Finance, Mr Dotto James, and interim Japanese Ambassador to Tanzania, Mr Katsutoshi Takeda, signed the exchange documents and grant agreement in Dar es Salaam yesterday.

Mr James explained that the support had come at a very critical moment when the government was in the process of reviving TAFICO, a project that ranks high in the development agenda, which seeks to improve the social-economic well-being of the citizens.

"Under this project, the following equipment will be supplied: fishing vessel (A multi-purpose fishing vessel with trawl gallows for stern trawlers, with the ability to freeze at least five days of fishing trips), ice making machine, cold room storage, fishing gear," he explained, adding:

"Others are tools for workshop marine (lLather machine, presser), refrigerated vehicle and pickup vehicle for supplying fish."



**The support had come at a very critical moment when the government was in the process of reviving TAFICO, a project that ranks high in the development agenda.**
*– PS Dotto James*

Mr James said that successful implementation of the project would contribute significantly towards achieving the objectives of the country's Five Year Development Plan II, which, among other goals, aims to improve the performance of the fisheries sector and ultimately attract more Tanzanians to engage in it as their main income-generating activity.

Between 2012 and 2019, the government of Japan has provided a total of 451.31bn/- as grants and 891bn/- as soft loan for projects in Tanzania.

The growth rate of the fishing sub-activity was 9.2 per cent in 2018, which was higher than 8.4 per cent recorded in 2017, attributed mostly to proper management of fish hatcheries, including privately-owned ponds and increased demand for fish and fish products in the domestic and foreign markets.

Continues on Page 3

Scanned by CamScanner

# Ranchi Kongwa kuzalisha ndama 3,200

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

MENEJA wa Ranchi ya Kongwa, Raymond Lutege, amesema wamejiwekea malengo ya kuzalisha ndama 3,258 katika kipindi cha uzalishaji mwaka huu kutokana na majike wazazi 4,072 walionao.

Lutege amesema hadi sasa ndani ya miezi mitano ya utekelezaji wa bajeti hiyo, wamezalisha ndama 268, sawa na asilimia tisa ya lengo na upimaji mimba umefanyika na kuonyesha idadi ya majike 3,113 yanatarajiwa kuzaa.

Akizungumza na Nipashe juzi, meneja huyo alisema uzalishaji kwa kipindi cha miezi mitano umepungua kutokana na msimu wa upandishaji ulioanza Machi mwaka jana hadi Agosti.

"Uzalishaji utaanza kuongezeka kwa kasi kubwa kuanzia Januari hadi Juni kutokana na msimu wa upandishaji," alisema.

Aliongeza kuwa ranchi hiyo inaendelea kukabiliana na matatizo ya magonjwa mbalimbali hasa kipindi cha miezi mitano ya uzalishaji, ambapo wamechanja ng'ombe na mbuzi chanjo ya mapafu kulingana na kalenda ya udhibiti wa magonjwa.

Alisema ranchi hiyo ilipanga kuzalisha kondoo 258 kwa mwaka huu wa fedha kutokana na majike wazazi 287, hadi kufikia mwezi Novemba, walikuwa wamezaliwa kondoo 118 ambao ni sawa na asilimia 45 ya makisio.

Alisema pia walipanga kuzalisha nguruwe 260, kwa majike wazazi 28 kwa mwaka na hadi sasa wamezalisha 66 na vifo ni 13.

"Katika uzalishaji wa mbuzi, tulipanga kuzalisha 572, kwa majike wazazi 635, ndani ya miezi mitano ya uzalishaji tumezalisha mbuzi 112, sawa na asilimia 35 ya uzalishaji, mbuzi 92 wamechinjwa na 19, wameuzwa," alisema.

Scanned by CamScanner

# Ujio wa Serikali watoa fursa wafugaji kuku

**Rachel Chibwete,** Mwananchi
rchibwete@mwananchi.co.tz

**Dodoma.** Wafanyabiashara wa kuku soko la Majengo wamesema ujio wa makao makuu Dodoma, umeleta neema kwao kwa kuwa sasa wanauza kuku wengi kuliko zamani.

Akizungumza jana na *Mwananchi* mwenyekiti wa wauza kuku sokoni hapo, Balozi Ngowe alisema biashara ya kuku sasa ni nzuri tofauti na zamani kwa kuwa walikuwa wanauza kuku si zaidi ya 10, lakini sasa wanauza kati ya 40 na 50 kwa siku.

Ngowe alisema wateja wakubwa wa kuku ni watu wa kawaida na wenye majiko ya kuchoma kuku jijini hapa ambao hununua wengi tofauti na ilivyokuwa kabla ya Serikali kuhamia Dodoma.

Naye katibu wa machinjio ya kuku sokoni hapo, Abuu Hamisi alisema idadi ya kuku wanaochinjwa kwa siku hutegemeana na biashara kwa siku hiyo.

"Kwa wastani tunaweza kuchinja kuku kati ya 1,500 hadi 2,000 kwa siku na gharama ya kuchinja kuku mmoja ni Sh500, lakini idadi hiyo inaweza kupanda au kushuka kutokana na wingi wa wateja siku hiyo," alisema.

Akizungumzia hali hiyo, meneja wa baa ya Tango, Aaron Isack alisema biashara ya kuku kwenye baa yake kwa sasa ni nzuri kwa kuwa awali alikuwa anauza chini ya 10 lakini kwa sasa anauza zaidi ya 50 kwa siku kutokana na wingi wa watu waliohamia Dodoma.

Scanned by CamScanner

# Japan yasaidia uvuvi

Aurea Simtowe, Mwananchi
asimtowe@mwananchi.co.tz

**Dar es Salaam.** Serikali ya Japan imeipatia Tanzania msaada wa dola 1.818 milioni za Kimarekani (sawa na Sh4.2 bilioni) kwa ajili ya kufufua Shirika la Uvuvi Tanzania (Tafico).

Mkataba wa makubaliano kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo umesainiwa jana ambapo umetajwa kuwa utasaidia kupunguza umasikini na kuwavutia Watanzania wengi kuingia katika uvuvi na kufanya kuwa shughuli kuu ya kujipatia kipato.

Akizungumza mara baada ya kusainiwa kwa mkataba huo, Kaimu Balozi wa Japan, Katsutoshi Takeda alisema kupitia fedha hizo meli kubwa kwa ajili ya uvuvi itanunuliwa na itakuwa na vifaa vya kisasa pamoja na mashine ya kutengeneza barafu.

"Lakini pia litatengenezwa ghala la baridi kwa ajili ya kuhifadhia samaki, vifaa mbalimbali vya kuvulia samaki na vya karakana vitanunuliwa. Pia gari lenye mtambo maalumu ya barafu na gari la kusambazia samaki vyote vitanunuliwa," alisema Takeda.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk Rashid Tamatamah alisema wanatarajia shirika hilo litaanza kufanya kazi Februari 2020 ikiwa ni baada ya utaratibu wa kisheria kukamilika.

"Tumeshaandaa waraka ambao utapelekwa katika vikao vya Bunge vitakavyofanyika Januari mwakani na kama litaridhia kurejeshwa kwake basi Februari litaanza kufanya kazi," alisema Dk Tamatamah.

"Tumekataa misaada mingi kutoka sehemu mbalimbali ambayo ilikuwa na masharti hasi lakini Japan wamekuwa wakitupatia misaada isiyokuwa na masharti hayo ndiyo maana tumekuwa tukiipokea."

Doto James

Naye Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Dotto James alisema nchi ya Japan imekuwa ikisaidia Tanzania katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo, tangu mwaka 2012 mpaka sasa misaada iliyotolewa na nchi hiyo ina thamani ya Sh452.31 bilioni.

"Tumekataa misaada mingi kutoka sehemu mbalimbali ambayo ilikuwa na masharti hasi lakini Japan wamekuwa wakitupatia misaada isiyokuwa na masharti hayo ndiyo maana tumekuwa tukiipokea.

"Hata mikopo wanayotupatia ni ya riba nafuu ambayo mpaka sasa

Scanned by CamScanner

